



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA KWIMBA



TANGAZO

TANGAZO LA UTOAJI TIBA KINGA YA POLIO ITAKAYOTOLEWA KWA NJIA
YA MATONE KWA WATOTO WENYE UMRI CHINI YA MIAKA MITANO
KUANZIA TAREHE 18 MEI HADI TAREHE 21 MEI, 2022

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya Kwimba anawatangazia Wananchi wote kuwa utafanyika utoaji wa Tiba Kinga ya Polio itakayotolewa kwa njia ya matone kwa watoto wenye umri chini ya Miaka mitano.

Zoezi hili litakuwa la nyumba kwa nyumba ambapo wataalamu wa Afya watapita kila nyumba yenye mtoto wa umri chini ya miaka mitano.

Wananchi wote mnaombwa kutoa ushirikiano kwa wataalamu watakaofika kwa kila kaya.

Wito unatolewa kwa walezi wote wawaandae watoto na wawepo katika kaya zao ili kuondoa usumbufu kwa watoa huduma watakaofika kwa ajili ya kutoa matone ya Polio. Wanafunzi walioko mashuleni huduma itatolewa shuleni.



"MPATIE MWANAO TIBA KINGA KWA MASLAHI YA TAIFA"

.....

H.J. MSANGA
MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA YA KWIMBA

*MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA YA KWIMBA*